KUSHEHEREKEA UTAKATIFU

JINSI YA KUANZA KUNDI NDOGO

CHURCH OF THE NAZARENE - AFRICA REGION

www.africanazarene.org

Je, Kundi Ndogo Ni Nini?

Kundi ndogo kanisani linamaanisha kundi la watu (3-12) wanaokutana mara kwa mara kwa nia ya kukua katika kumjua na kumfuata Kristo. Nia ya kundi ni kuamua hali ya kundi, ushirika na mazoezi.

Je, Kusudi la Kundi Ndogo ni lipi?
Washiriki hukutana katika kundi ndogo ili kushiriki katika Maombi na Kufunga, Mafundisho ya Biblia na katika uhusiano wa Maagano na Uwajibikaji kwa Mungu na Kanisa na pia kwa watu binafsi na pia katika umoja wa kusheherekea utakatifu.

Kusudi la mwisho la vikundi vidogo vya {Kusherehekea Utakatifu} kuendelea kuwa shirika takatifu la Kikristo, lililotakaswa kamili, likitafuta kuokolewa kwa wenye dhambi, kujengwa kwao katika utakatifu na kutafuta urahisi na kudhihirishwa kwa nguvu za kiroho katika Kanisa la kale la Agano Jipya. (*Kitabu cha Mwongozo Manual 2009-2013, Aya ya 25*)

Jinsi Ya Kuanza Kundi Ndogo

- Amua aina ya kundi unalotaka kuanzia kulingana na kusudi lililotajwa
- ambalo ni Maombi na Kufunga, Mafundisho ya Biblia, Kundi lenye maagano na Uwajibikaji?

ha

- Je, washirika ni nani? Je, mtu ye yote anaweza kujiunga, au ni la watu fulani? Idadi ya watu katika kundi itatoa ushawishi wa kuwa karibu na uwazi.

- Je, kundi litakuwepo kwa muda gani? Wakati wa uanzilishi au zaidi (3½ hadi miezi sita ama zaidi)

- Je, kila kipindi kinachukua muda wa kiasi gani? Saa 1 – 1 ½

- Imarisha ni makundi ngapi madogo ambayo ungependa kuanzisha.
- Ni makundi ngapi ambayo yameundwa katika ushirika.
- Kadiria mahali walipo, uwezo wao, na jinsi wanavyoleta matokeo ya malengo waliyoweka. Chukulia hii kuwa fursa ya kurejelea, na kuanzisha upya. Kulingana na idadi ya Wakristo na uwepo wa viongozi waliojitolea, kiwanga cha makundi matatu ama manne yanapendezwa badala ya kundi moja.

- Tafuta vifaa vilivyopendekezwa ili kusaidia kundi ili kutimiza malengo yake. Hakikisha kuwa vifaa vyote vimeidhinishwa na Mchungaji kabla ya kutumika. Orodhesha wasaidizi kama wenyeji, viongozi wenza, na kadhalika. Inapendekezwa kuwa wenyeji hawafai kuhudumu kama viongozi wa kundi. Chagua mahali pa mkutano, andaa mipango inayofaa ili kutayarisha kwa matumizi.
- Tangaza na utoa mwaliko. Toa habari nyingi uwezavyo hasa kuhusu kusudi la mkutano, mazoezi yatakayofanyika, mahali, wakati, uongozi na ushirika.

- Masharti ya ushirikia yanajumlisha:
- Hamu na njaa ya utakatifu.
- Kujitolea nafsi kukutana mara kwa mara wakati fulani.
- Kujitolea nafsi katika kuleta mazingira yenye usalama ya usiri.
- Moyo wakutambua na kufurahia manufaa yao ya kushiriki katika kundi ndogo kama:
- Fursa ya kujifnza kwa kama Kristo.
- Sehemu zenye usalama ambapo watakua kiroho na kuwa kama Kristo.
- Hisia ya ujamaa.

- Punde tu aina ya kundi itakapoamuliwa, maagano yaliyowazi na hatua za uwajibikaji zitaanzishwa na Wakristo wote watahitaji kujitolea.

- **Jukumu la Kiongozi wa Kundi Ndogo**

- Kuongoza mkutano na kuhakikisha kuwa kundi linatimiza lengo lake. Ili kuhakikisha jambo hili linatimia mambo yafuatayo yanafaa kuhusishwa:
- kujiandaa kabla ya mkutano.
- Kufuata agenda
- Kuanza na kukamilisha vikao kwa wakati unaofaa ili kuepuka mambo yatakayoadhiri mipango ya wenyeji ama washirika.

- **Kupokea maarifa ya kuongoza kundi itajumlisha mambo kama vile:**
- Upendo thabiti. Kuonyesho upendo usio na masharti na kumpokea kila mshiriki kama alivyofanya Kristo.
- Kusikiza na kukubali kwa kuhisi maono yao.
- Hakikishia msemaji kuwa mawazo na hisi zake zimesikizwa na zimeeleweka vyema.
- Kuomba msaada. Kuwa tayari kukubali wakati ambapo hamna jibu, na kuomba msaada wa kundi.
- Kuanzisha njia ya kuuliza maswali ambayo itawahimza washiriki kufikiria na kujadili. Tumia maswali yaliyo na rahisi yenye maneno kama vile nani, nini, lini, kwanini, wapi na vipi. Subiri majibu yao.
- Epuka hali yeyote ambayo italeta fedheha kwa mtu yeyote asiye na jibu.

- Ili kupokea maarifa ya shughulikia hali tata zinazoguza utu tofauti tofauti, kukosa mwelekeo, masengenyo ambayo huja kama ombi na kadhalika. Shughulikia mambo haya yote kwa njia ya umaarufu.

- Kumtegemea Mungu ili kudumisha na kusaidia kundi kufikia lengo lake. Ni vizuri kuweka mipango lakini kuwa tayari kuwacha mapenzi ya Mungu yafanyike.

- **Utaratibu wa mambo ya kufanya katika Kundi Ndogo**

- **Kuomba na Kufunga**

  - **Dakika 15**: Kuimba na kutoa ushuhuda kwa maombi yaliyojibiwa. Mara kwa mara angalia orodha ya maombi.

  - **Dakika 15**: Soma maandiko lakini usihubiri wala kufundisha.

  - **Dakika 30:** Kwa kifupi shirikiana mambo yanayohitaji maombi kulingana na mipango maombi ama kusudi la kundi, chukua mda wa maombi.

- **Mafundisho ya Biblia**

  - **Dakika 15:** Kwa kifupi ongoza ushirika kufuatiwa na maombi na wimbo wa kufungua.

  - **Dakika 30**: Soma sehemu ya mafundisho, na kujadili kwa kutumia maswali fulani ili kusaidia katika kupata lengo la kipindi hiki. Jaribu kuelewa: Je, mafundisho haya yanatuambia nini, maanake ni nini, jinsi inavyoweza kutumika hapa na sasa. Jaribu kuhusisha washirika katika majadiliano.

  - **Dakika 15**: Kwa kifupi shiriki mambo yanayohitaji kuombewa na mahitaji ya kibinafsi ambayo yametokea kufuatia majadialiano. Tumia mda katika maombi. Kila wakati fuatilia mambo ambayo yametajajwa yanayohitaji maombi.

  - **Maagano Na Uwajibikaji (uhusiano wa Mungu Na Kanisa)**

  - Kundi Ndogo pengine litaanzishwa ikiwa kunayo haja kuu ya kutembea na Mungu.

- Imba wimbo/tambio fupi na kufungua kwa maombi.
- Fuata kwa maswali ya uwajibikaji kama ilivyokubalika, mfano
- Hali ya moyo wako ni ipi?
- Je, unafanya nini ili kujisaidia kukua kiroho?
- Je, ulikuwa na fursa gani juma hili kuwahudumia watu wengine, na ulizitumia fursa hizi vipi?
- Je, ulipatwa na majaribio yapi, na uliyashinda vipi?
- Kwa kifupi mambo ambayo yanahitaji maombi kisha kuombeana. Kila wakati fuatilia mambo ambayo yametajwa na yanahitaji kuombewa.

Nakala hii imetayarishwa na
Kasisi Daphne Mathebula,
Mkurugenzi Mkuu wa SDMI Eneo La Africa